MAWASILIANO - Angalia na uombee vituo vya mawasiliano na vituo vya radio, vituo vya runinga wachapishaji magazeti. Ombea Hadithi ya Mungu na ushuhuda ya wafuasi wake viweze kusambazwa kote mjini na kote duniani. Omba kwamba ujumbe wake unaweza kuwasilishwa kupitia wajumbe hadi kwa umati na kwamba watu wa Mungu kila mahali wataona kazi yake.

KIROHO - Angalia na ombea vituo vya Kiroho kama vile majengo ya kanisa, majengo ya miskiti ama hekalu. Omba kwamba kila mtafutaji wa kiroho atapata amani na faraja kwa Yesu na wasiweze kuvutwa ama kuchanganyishwa na mafundisho ya dini ya uongo.

UTENDAJI [Dakika 60-90] - Mkajigawanye kwa vikundi vya watu wawili ama watatu na mkaende nje kwa jamii mkijizoeshe kutembea kwa maombi. Kuchagua mahali inaweza kuwa rahisi kama vile kutembea kutoka kwa kikao ama kutembea kwa maombi na kupangia mahali. Nenda jinsi Mungu anavyoongoza, na upange kutumia dakika 60-90 katika utendaji huu.

FAHAMU - Hakikisha umejifunza na kujizoesha maombi ya B.A.R.A.K.A. Hapa chini kabla uondoke.

Maombi ya B.A.R.A.K.A

Mwisho, hapa kuna njia tano unaweza kuwaomba watu unaokutana nao wakati wa Kutembea kwa Maombi:

Unapotembea na kuomba, kuwa macho kwa fursa na usikize maongozi ya Roho wa Mungu kuomba watu binafsi na vikundi unayokutana navyo njiani.

Unaweza kusema, "Tunaomba jamii, je, kuna kitu tunachoweza kuwaomba kukihusu?" Ao sema, "Ninaomba eneo hili. Je kuna kitu maalum mnahitaji niombee?" Baada ya kusikia majibu yao unaweza kuwauliza kuhusu mahitaji yao wenyewe. Wakizishiriki, waombee mara moja. Ikiwa Bwana ataongoza,

unaweza kuombea mahitaji mengine pia.

Tumia neno B.A.R.I.K.I kukusaidia njia 5 ambazo unaweza kuomba:

- Mwili [afya]
- **Kazi** [kazi na fedha]
- **Hisia** [maadili]
- **Kijamii** [mahusiano]
- **Kiroho** [kujua na kumpenda Mungu zaidi]

Kwa hali zingine, watu wanashukuru unajali zaidi hata kuwaombea.

Ikiwa mtu yule si Mkristo, maombi yako yanaweza kufungua mlango wa mawasiliano kiroho na fursa yako kushiriki hadithi yako na hadithi ya Mungu. Unaweza kuwaalika kuwa sehemu ya wasomi wa Biblia au hata uende kwa nyumba ya mmoja wao.

Ikiwa mtu yule ni Mkristo unaweza kumualika aungane nawe katika kutembea kwa maombi ama au uwafundishe jinsi wanaweza kutembea kwa maombi na kutumia hatua rahisi kama kuombea sehemu za ushawishi au B.A.R.I.K.I. Maombi ya kufanya jamaa ya Mungu kukua zaidi. .

UTENDAJI [Dakika 15] - Mkajigawanya kwa vikundi vya watu wawili au watatu na mkatumie dakika 15 mkijizoeza maombi ya B.A.R.I.K.I. Jizoeshe kuombea maeneo 5 ya B.A.R.A.K.A. Ombea mtu NA ukajizoeashe jinsi unaweza kufundisha watu kuelewa na kutumia maombi ya B.A.R.A.K.A.

KIPINDI CHA 06

Katika kipindi hiki, tutajifunza jinsi Mungu anavyotumia wafuasi waaminifu – hata kama bado ni wapya kabisa – zaidi ya wale walio na hekima ya miaka na mafunzo ambayo hawawezi kutii. Na tutaangalia kwa mara ya kwanza njia ya kukutana pamoja ambayo husaidia wanafunzi kujizidisha kwa haraka.

Muundo wa Vikundi vya Theluthi 3/3

Yesu alisema -- “walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.”

Hiyo ni ahadi yenye nguvu, na ambayo kila mfuasi wa Yesu anastahili kuuchukua kwa ubora unaostahili. Lakini mkija pamoja kama kundi, mnastahili kutumia wakati wenu aje?

Kundi la theluthi 3/3 ni lile ambalo hugawanya wakati wao pamoja kwa sehemu 3, ili waweze kujizoeshia kutii mambo mengine muhimu yanayoamuriwa na Yesu.

Hivi ndivyo inavyofanya kazi:

ANGALIA NYUMA [Theluthi 1/3 ya wakati wako]

Utunzi na Maombi: Kila mtu apewe wakati wa kushiriki kitu anachotoa shukrani kwacho. Kisha kila mtu ashiriki kitu kile wanapambana nacho. Acha mtu aliye upande wa mkono wa kulia aombe vitu vile ameshiriki. Ikiwa mtu anapambana na kitu ambacho kinahitaji uangalizi zaidi, baki nyuma ukamhudumie mtu yule.

Maono: Tumia wakati wenu kuimba pamoja na kufunganisha mistari na mandhari ya Mungu mwenye mapenzi, kupenda wengine, kumshirikisha Yesu na wengine, kuanzisha vikundi vipya, na kuwasaidia wengine kufanya vivyo hivyo. Vinginevyo watu wanaweza kushiriki vifungu vya Biblia vinavyowasiliana kuhusu mandhari hizi.

Tia alama: Kila mtu ashiriki jinsi alivyojihusisha katika ahadi alizoandika kutoka juma liliopita:

1. Umetii aje yale ulijifunza?
2. Umefundisha nani kutokana na yale uliyojifunza?
3. Umesiriki na nani hadithi yako ama hadithi ya Mungu?

Ikiwa walisahau kufuatilia ahadi ama hawakuwa na fursa ya kufanya hivyo, basi hizo ahadi za juma lililopita ziongezwe kwa ahadi ya juma hili. Ikiwa mtu atakataa kutii kitu alichokisikia wazi kutoka kwa Mungu basi na ichukuliwe kama suala la nidhamu kanisani..

ANGALIA JUU [Theluthi 1/3 ya wakati wako]

Omba: Ongea na Mungu kwa urahisi na kwa ufupi. Omba Mungu akufundishe kifungu hiki.

Soma na Mkajadili: Soma kifungu cha juma hili. Jadilianeni maswali haya

1. Ulipenda nini kuhusu kifungu hiki?
2. Ulipata changamoto ipi ama kilichokuwa kigumu kuelewa kuhusu kifungu hiki?

Soma kifungu cha juma hili tena.

3. Tunaweza kujifunza nini kuhusu watu katika kifungu hiki?
4. Tunaweza kujifunza nini kuhusu Mungu kutoka kifungu hiki?

ANGALIA MBELE [Theluthi 1/3 ya wakati wako]

Tii. Fundisha. Shirikiana. : Tumia dakika tano kwa maombi ya ukimya. Acha kila mtu katika kundi aombe Roho Mtakatifu awaonyeshe jinsi ya kujibu maswali, kisha waweke ahadi. Kila mtu anastahili kuandika ahadi hizo ili waweze kuomba watu kwa hekima na kuwafanya waajibike. Huenda hawatasikia kitu kuhusiana na kila swali kila juma.

Wanastahili kuandika ikiwa wanashiriki jawabu wasilokuwa na hakika walilisikia kutoka kwa Mungu, lakini wanafikiri inaweza kuwa wazo nzuri kwa kuwa uwajibikaji utashughulikiwa kwa ngazi tofauti.

5. Je naweza kutumia na kutii kifungu hiki?
6. Nitamfundisha nani ama kushiriki naye kuhusu kifungu hiki?
7. Ni nani Mungu anataka nishiriki naye hadithi yangu [ushuhuda] na/au hadithi ya Mungu juma hili?

Jizoeshe: Katika kikundi cha wawili ama watatu, mkajizoeshe kile mmeahidi kufanya katika swali la 5, 6 ama

7. Kwa mfano, Jukumu ya kucheza ni mawasiliano magumu ama kukabiliana na majaribu; jizoeshe kufundisha kifungu cha leo, au kujizoesha kushiriki Injili.

Ongea na Mungu: Katika vikundi hivyo hivyo vya wawili ama watatu, ombea kila mwanachama mmoja mmoja. Na ukamuulize Mungu kutayarisha moyo ya watu watakaokuwa wanasikia kuhusu Yesu juma hili. Muulize akupe nguvu na hekima ya kuwa mtiifu kwa ahadi zako. Huu ndio mwisho wa mkutano.

Baada ya kila mmoja kumaliza, mkashiriki Meza ya Bwana au mle chakula pamoja.


FAHAMU – Kuna baadhi ya vifungu vilivyopendekezwa ambapo vikundi vyenu vya theluthi 3/3 vinaweza kujisomea katika Kiambatisho cha Kitabu cha Mwongozo

KIPINDI CHA 07

Katika kipindi hiki, tutajifunza Mfuatano wa Masomo ambayo husaidia wanafunzi kwenda kutoka kwa mmoja hadi kwa wengi na kugeuza umisheni kuwa harakati. Pia tutajzoesha muundo wa vikundi vya theluthi 3/3 na kujifunza jinsi mnavyokutana kunaweza kusaidia njia mnayojizidisha.

Mfuatano wa Mafundisho

Mfuatano wa Mafundisho ni Mfano, Msaada, Angalia na Kuacha, na hufanya kazi hivi:



MFANO – Mfano ni kuwa kilelelezo cha chombo cha kujizoeshwa. Ndio sehemu fupi ya mfuatano wa mafundisho. Kwa kawaida inahitaji kufanywa mara moja tu. Ni kuleta hamasisho kwamba kujizoeshwa ama chombo kipo na hutoa maoni jinsi ilivyo. Kuwa mfano mara kwa mara sio njia bora kuandaa mtu. Wanahitaji kuruhusiwa wajaribu ustadi wao wenyewe.

Wakati mtoto atakapona mtu akiendesha baiskeli, hiyo ni sura ya MFANO.

KUSAIDIA – Kusaidia ni kumruhusu mwanafunzi ajizoeshwa kwa ustadi wake. Huu huchukua muda mrefu kuliko sura ya mfano. Inahitaji “kushikiliwa” upande wa mshauri. Mshauri anahitaji kuwa mwelekezi na kuchukua jukumu la kufundisha mwanafunzi. Awamu hii haikai kwa muda mrefu hadi mwanafunzi awe na uwezo kamili, lakini wameelewa misingi ya ustadi. Awamu hii ikiendelea kwa muda mrefu, hivyo mwanafunzi atamtegemea sana mshauri na hataendelea hadi awe na uwezo kamili. Mwisho wa awamu unastahili kuwekewa alama na mwanafunzi anayeanza kuwa mfano kwa wengine.

Wakati mzazi anaposhikilia baiskeli mtoto akijifunza kuiweka sawa, hiyo ni awamu ya KUSAIDIA.

ANGALIA – Kuangalia ndio awamu ndefu sana. Ina husisha mawasiliano yasiyo ya moja kwa moja na mwanafuzi. Inatafuta kuendeleza uwezo kamili katika nyanja zote za ustadi. Inaweza kuwa mara kumi ama zaidi bora tu zile awamu mbili zimeunganishwa. Wakati mwanafunzi anaendelea kupata ujuzi, kuonana na mshauri utapungua kwa kusudi maalum. Katika awamu hii mwanafuzi anawajibika zaidi na mvumbuzi katika utendaji wa ujuzi. Kwa kawaida katika kufanya wanafunzi mwisho ya awamu hii wakati mwanafunzi atakuwa amewapa kizazi cha nne ustadi wake aliokuwa akijifunza.

Wakati mzazi anapoangali mtoto akiendesha baiskeli na kuhakikisha wana ustadi na ujuzi ya kutosha bila kutazamwa, hii ni awamu ya KUANGALIA.

ACHA – Kuacha ni kama kufuzu wakati mwanafunzi anapokuwa mshauri mwenzio. Mawasiliano ya mara kwa mara na kuwa mshauri utaendelea ikiwa mwanafunzi na mshauri na wako kwa mtandao moja.

Wakati mzazi anamruhusu kuendesha abaiskeli bila kuangaliwa, hiyo ndio awamu ya KUACHA.

Jizoeshe Theluthi 3/3 ya Vikundi

UTENDAJI [Dakika 90] – Acha kundi lako litumie dakika 90 kujizoesha theluthi 3/3 ya Vikundi ukitumia sehemu ya theluthi 3/3 ya vikundi katika ukurasa wa 19-20.

- **ANGALIA NYUMA** – Tumia Changamoto ya Kikao cha juma lililopita kujizoesha “Uaminifu”
- **ANGALIA JUU** – Tumia Marko 5:1-20 kama kifungu cha kundi lako kusoma kisha ujibu maswali - 4
- **ANGALIA MBELE** – Tumia maswali 5, 6, na 7 kuendeleza jinsi utakavyo tii, utakavyofundisha na kushirikiana

KUMBUKA – Kila sehemu inapaswa kuchukua 1/3 [au dakika] ya wakati wenu wa kujizoesha.

KIPINDI 08

Katika kipindi hiki, tutajifunza jinsi Chembe ya Uongozi huandaa wafuasi kwa muda mfupi kukua viongozi wa maisha. Tutajifunza kwa nini kuhudumia wengine ni mkakati wa uongozi wa Yesu. Na tutatumia wakati wetu tukijizoeshwa kama kundi la theluthi 3/3, tena.

Chembe za Uongozi

Chembe za Uongozi ni Kundi la 3/3 ambayo hukutana kwa muda mfupi wakati ulioamiziwa. uliowekwa kabla ya uamuzi [kama vipindi hivi – 9 Kosi za Mafundisho ya Zúme]. Kusudi ni kuandaa kundi la watu kuenda nje na kuanzisha vikundi vyao ama waanzishe chembe nyingine ya uongozi wakati wanamalizia mafundisho yao.

Njia hii inaweza kutumika katika hali kadhaa. Inaweza kutumika na kiungo cha jamaa wa kuhama hama kama vile wanafunzi, nk. Inaweza kutumika ikiwa idadi ya watu ambao tayari ni Wakristo na kwa sababu zingine haifai kwao kuunda kundi linaloendelea na wanahitaji kufundshwa jinsi ya kuanzisha kundi lao wenyewe. Inaweza pia kutumika ikiwa kuna hali ambapo idadi kubwa ya watu wanaokoka kwa wakati moja na hakuna wakati wa kutosha au fursa ya kufanya ufuatiliaji wa moja kwa moja na Baraka Kuu au njia kama hiyo.

Jizoeshe Theluthi 3/3 ya vikundi, tena

UTENDAJI [Dakika 90] – Acha kundi lako litumie dakika 90 mkijizoeshwa theluthi 3/3 ya vikundi mkitumia mfano wa theluthi 3/3 katika sehemu ya vikundi, katika ukurasa wa 19-20.

Wakati huu:

- **ANGALIA NYUMA** – Tumia Kutii, Kufundisha, na Kushirikiana kwa kipindi kilichopita na mkashirikiane changamoto zenu kwa kujipima kwa kila mmoja.
- **ANGALI JUU** – Tumia Matendo 2:42-47 kama kifungu cha kundi lako kusoma kisha mkajibu maswali 1- 4
- **ANGALIA MBELE** – Tumia maswali 5, 6, na 7 kuendeleza jinsi utakavyo tii, utakavyofundisha na kushirikiana.

Badilisha uongozi kwenye kundi katika kipindi chote ili kila mmoja awe na nafasi ya kuongoza, au kuomba, au kuuliza maswali. Himiza na kufundisha kila mmoja kuhusu kinachoendelea sawa, kinachoweza kuwa bora zaidi na mazoezi ya muda mfupi, na kinachoweza kuwa kizuri kwa hatua inayofuata kwa kila mmoja wa wanafunzi kukua hata zaidi.

KUMBUKA- Kila sehemu inastahili kuchukua kama 1/3 [au dakika 30] ya wakati wenu wa kujizoeshwa.

KIPINDI CHA 09

Katika kipindi hiki, tutajifunza jinsi muundo wa mstari huzuia ukuaji wa ufalme na jinsi Mafikira Yasiyofuatana hukusaidia kuzidisha wanafunzi. Tutagundua jinsi wakati unafaa katika kufanya-wanafunzi na jinsi ya kuzidisha mwendo wetu. Tutajifunza jinsi wanafunzi wa Yesu wanaweza kuwa Sehemu ya Mekanisa Mawili kusaidia kugeuza jamaa wenye imani na wa kiroho kuwa mji mkubwa unaokua wa waumini. Hatimaye, tutajifunza jinsi Mpango rahisi wa miezi 3 unaweza zingatia jitihada zako na kuzidisha ufanisi wako wa kufanya jamaa ya Mungu kukua kwa haraka.

Mpango wa Miezi - 3

Kwa vile sasa umejulishwa kwa chombo cha msingi wa ufanyaji wa wanafunzi, tumia wakati wako kwa maombi na mwulize Mungu hasa kile angependa ufanye kwa miezi mitatu ijayo. Ukishatumia muda wako kumsikiliza, jaza mpango ufuatao. Shirikiana mpango wako na mwenzako na uanzishe ratiba ya ufuatiliaji ya uajibikaji ya wakati mtakapotembeleana majuma 1,2,3,4,6,8, na 12, kutoka sasa.

Nitashiriki Hadithi Yangu [Ushuhuda] na Hadithi ya Mungu [Injili] na wafuatao:

Nitaalika watu wafuatao ili kuanzisha Kundi la Uajibikaji pamoja nami:

Nitawapa wafuatao changamoto wakaanzishe Vikundi vyao vya Uajibikaji na kuwafundisha jinsi ya kufanya:

Nitaalika watu wafuatao kuanzisha Kundi la theluthi 3/3 pamoja nami:

Nitawapa wafuatao changamoto wakaanzishe Vikundi vyao vya theluthi 3/3 na wakawafundishe jinsi ya kufanya:

Nitaalika watu wafuatao wakashiriki katika theluthi 3/3 Tumaini au Kundi la Uvumbuzi [angalia kiambatisho]:

Nitaalika watu wafuatao wakashiriki kwa maombi ya kutembea pamoja nami:

Nitawezesha watu wafuatao kushiriki hadithi zao na Hadithi ya Mungu na kutengeneza orodha ya watu 100 katika mtandao wao wa mawasiliano:

Nitawawekea watu wafuatao changamoto wakatumie chombo cha mfuatano wa Maombi mara kwa mara:

Nitatumia chombo cha Mfuatano wa Maombi mara moja kwa _____[masiku / juma / miezi].

Nitafanya Maombi ya Kutembea mara moja kila _____[masiku / juma / miezi].

Nitaalika watu wafuatao kuwa sehemu ya Chembe cha Uongozi nitakalokuwa nikiongoza:

Nitawahimiza watu wafuatao Wakajifunze Masomo ya Zúme:

Maoni Mengine:

MAFUNDISHO YA JUU KIPINDI CHA 10

Katika kipindi hiki cha masomo ya Juu, tutajifunza jinsi tunavyoweza kuimarisha Uwezo wetu wa Kufundisha na orodha ya tathmini ya haraka. Tutajifunza jinsi Uongozi katika Mtandao huwezesha ukuaji wa makanisa madogo kufanya kazi pamoja ili kutekeleza zaidi. Na tutajifunza jinsi ya kuendeleza Vikundi vya Ushauri ambavyo huwapeleka viongozi katika ngazi mpya ya uongozi.

Orodha ya Kufundisha

Orodha ya Kufundisha ni chombo muhimu chenye nguvu unachoweza kutumia kwa haraka kuchunguza uwezo wako mwenyewe na udhaifu unapofikia kufanya wanafunzi ambao wanajizidisha. Pia ni chombo muhimu unachoweza kutumia kusaidia wengine – na wengine nao wanaweza kutumia kukusaidia

Tumia hatua zifuatazo kukamilisha hii tathmini binafsi [dakika 5-au chache]:

- **HATUA YA 1** – Soma Chombo cha Mafundisho cha Wanafunzi kilicho upande wa kushoto wa orodha yako.
- **HATUA YA 2** – Weka alama kwa kila chombo cha mafundisho, ukitumia taratibu inayofuata:
 - Ikiwa hujui ama huelewi Chombo – weka alama kwa safu NYEUSI
 - Ikiwa unafahamu lakini huna uhakika kuhusu Chombo – weka alama kwa safu NYEKUNDU
 - Ikiwa unaelewa na huwezi kufundisha vya msingi wa Chombo – weka alama kwa safu ya MANJANO
 - Ikiwa unajihisi uko na ujasiri unaweza kufundisha Chombo – weka alama kwa safu ya KIJANI

KUMBUKA- Hakikisha meshirikisha rodha yako ya matokeo ya Mafundisho na mwalimu wako au mwenzako ama mshauri mwingine. Ikiwa unasaidia kufundisha ama kushauri mtu, shirikisha chombo hiki ili kusaidia kutathmini maeneo yanayohitaji utumishi wako na mafundisho.

ORODHA YA KUSAHIHISHA MAFUNDISHO

- BLACK:** Wafundishe habari mpya na kuhakikisha wameelewa.
- RED:** Acha na ukae nao hadi wameelewa vya kimsingi.
- YELLOW:** Jihadhari na ushindani thabiti.
- GREEN:** Achana nao katafute wengine ukawastawishe.

CHOMBO CHA MAFUNDISHO

	MFANO	SAIDIA	TAZAMA	ONDOKA
	HAJUI	BILA UJUZI	UWEZO	MWENYE UJUZI
	Wajibu wa Mkufunzi			
	Mkufunzi Anapeana Mwelekeo na Habari	Mkufunzi Anapeana Mwelekeo & Msaada	Mkufunzi Anapeana Msaada & Himizo	Mkufunzi anapokea uboresho
	Jinsi Mipango Zinavyotengenezwa			
	Mkufunzi anaamua	Mkufunzi/ee Jadili Mkufuzi anaamua	Mkufunzi/ee Jadili Mwanafunzi anaamua	Mwanafunzi anaamua
Wanafunzi Wanaotumbukiza				
Simulia Hadithi yako [Ushuhuda]				
Simulia Hadithi ya Mungu [Injili]				
Msimamizi wa Mahusiano – Orodha ya 100				
Kasi				
Huduma Isiyo na-Mtiririko				
Muundo wa Kundi la Theluthi 3/3				
Simple Church – Penda Mungu/Wengine, Fanya Wanafunzi				
Kuwa sehemu ya Mekanisa Mawili				
Mzunguko wa Mafundisho				
Kundi la Uwajibikaji				
Kujilisha-Binafsi:				
• Soma Neno la Mungu Kila Siku [Tii]				
• Omba – Ongea & Usikize [Mzunguko wa Maombi]				
• Mwili Uhai - Ushirika [La Mwingine]				
• Dhuluma & Kuteseka				
Macho ya kuona kule Hakuna Ufalme				
Kumtafuta Mtu wa Amani [Mt. 10 Lk. 10]				
Maombi ya Kutembea				
Kuwa Kanisa:				
• Ushirika [Mle Pamoja, La Mwingine]				
• Sifa & Ibada				
• Biblia [Tii, Fundisha]				
• Kuwaelezea Watu Kumhusu Yesu [Shirikisha]				
• Ubatizo				

Vikundi vya Ushauri

Yesu alisema - "Amri mpya nawapa: Mpendane. Kama vile nilivyowapenda, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi."

Kundi la ushauri ni kundi ambalo lina watu ambao wanaongoza na kuanzisha Vikundi vya theluthi 3/3. Pia linafuata muundo wa theluthi 3/3 na ni njia nzuri ya kutathmini afya ya kiroho ya kazi ya Mungu katika eneo lako.

Vikundi vya Ushauri hutumia ushauri wa kiongozi-kwa-kiongozi na wafuasi wa Yesu binafsi, na makanisa vivi hivi, au hata na mtandao wa kanisa ya kimataifa unaofikia kote ulimwenguni.

Washiriki wa Kundi la Ushauri wanaangalia viashiria vya lengo wakifuata mkakati wa Yesu wa huduma na kuuliza maswali na kutoa maoni. Vikao hivi havikuwa na maana ya kupuzilia ubinafsi wa mtu ama kufanya mtu ajihisi duni. Ni vya kufundisha na kuhamasisha.

Tumia muundo huu rahisi:

ANGALIA NYUMA [1/3 ya wakati wako]

Wakati wa theluthi ya kwanza - tumia wakati wako kwa maombi na uangalifu kama vile ingekuwa katika msingi wa kundi 3/3. Kisha tumia wakati kuangalia maono ya kundi na uaminifu katika ahadi za awali:

Je ni vipi unadumu kwa Kristo? [Maandiko, maombi, kuamini, kutii, muhimu sana uhusiano?] Je, kundi lako lilikamilisha kitendo chako, mpango wa kikao kilichopita? Zitaathmini.

ANGALIA JUU [1/3 ya wakati wako]

Acha kundi likajadili maswali rahisi yafuatayo:

1. Unafanya aje katika kila sehemu ya mchoro wa Uwanda wa Nne?
2. Kitu gani kinafanya vizuri? Changamoto zako kuu ni nini?
3. Kagua ramani ya sasa ya kizazi.
4. Ni kitu gani kilichokutia changamoto au ni kitu gani kilichokuwa kigumu kwako kuelewa?
5. Mungu amekuwa akikuonyesha nini hivi karibuni?
6. Je, kuna maswali kutoka kwa viongozi wa majira au washiriki wengine?

ANGALIA MBELE [1/3 ya wakati wako]

Tumia muda wako kwa maombi ya kimya na kila mtu katika kundi ukiuliza Roho Mtakatifu kuwaonyesha jinsi ya kujibu haya maswali:

7. Ni mipango gani au malengo Mungu angependa nitumie kabla ya wakati wetu pamoja? [Tumia chombo cha Uwanda wa Nne kukusaidia katika kazi yako.]

8. Je, mshauri wangu au Wanachama wengine wa Kundi wanaweza kunisaidiaje katika kazi hii?

Hatimaye tumieni wakati wenu kama kundi mkiongea na Mungu kwa maombi.

Acha kundi likaombe ili kila mmoja awe ameombewa na umuulize Mungu kutayarisha mioyo ya wale watakaofikiwa na kundi wakati watakuwa mbali mbali.

Omba kwamba Mungu ampe kila mwanachama wa kundi ujasiri na nguvu kutumia na kutii yale Mungu amewafundisha katika kipindi hiki. Ikiwa kiongozi wa majira anahitaji kuomba kiongozi mchanga, huu ndio wakati mwafaka wa ombi hilo.

Kwa kuwa makundi haya hukutana mara nyingi hukutana mbali mbali, hakuna uwezekano wa kusherehekea Meza ya Bwana ama kushiriki chakula pamoja, lakini hakikisha kutenga wakati kuwatembelea kuona hali zao za kiafya na jamaa na marafiki.

Mchoro Wa Shamba Nne



Shamba Linalojizalisha: ukiwa na nani, jinsi gani na wakati gani utachuja watu ili upate wale waaminifu na kuwapa uwezo na kuwafanya kuwajibikia uzalishaji?


Shamba Tupu: wapi ama na nani [kundi lipi la watu] umepangia kueneza Ufalme?

Shamba la kuweka mbegu: wapi au unashiriki habari njema za Ufalme na nani


Shamba lenye Kukua: unawapa watu uwezo kwa njia gani na kuwafanye wakue kiroho, mmoja mmoja na katika mtandao wao wa asili?

Shamba la Mavuno: Je, jamaa wapya wa kiroho [makanisa vivi hivi] yanapataje umbo?

Muundo wa Uakilishi Rahisi wa Kanisa kwenye Ramani ya Vizazi



Group



Kiambatisho

Safu ya Vikundi vya theluthi 3/3

SAFU LA TUMAINI [KWA WATAFUTAJI]

Tumia vifungu vifuatavyo kwa

“ANGALIA JUU” Sehemu ya kundi lako. Yawezekana kundi lako litahitaji zaidi ya mkutano moja kwa baadhi ya vifungu vingine.

1. Tumaini la mwenye dhambi: Luka 18:9-14
2. Tumaini kwa maskini: Luka 12:13-34
3. Tumaini kwa aliyetoroka: Luka 15:11-32
4. Tumaini kwa waliopotea: Luka 19:1-10
5. Tumaini kwa mwenye kuomboleza: Yohana 11:1-44
6. Tumaini kwa mtafitaji: Yohana 3:1-21

ISHARA ZA YOHANA [KWA WATAFUTAJI]

Tumia vifungu vifuatavyo kwa

“ANGALIA JUU” Sehemu ya kundi lako. Yawezekana kundi lako litahitaji zaidi ya mkutano moja kwa baadhi ya vifungu vingine.

1. Kugeuza maji kuwa divai: Yohana 2:1-12
2. Kumponya mwana wa diwani: Yohana 4:46-54
3. Kumponya aliyepooza: Yohana 5:1-17
4. Kulisha watu elfu tano: Yohana 6:1-14
5. Kutembea kwa maji: Yohana 6:15-25
6. Kumponya mtu aliyezaliwa kipofu: Yohana 9:1-41
7. Kumfufua Lazaro: Yohana 11:1-46

ANZA KUFUATILIA: MIKUTANO 8 ZA KWANZA

Hii inafaa kwa watu ambao tayari ni Wakristo lakini hawajawahi kuwa katika aina hii ya kundi Sehemu ya zoezi linaelekezwa na vikao hivi 8.

Kujiozea binafsi kulianza na mkutano ifuatayo.

1. ELEZEA HADITHI YAKO

ANGALIA JUU: Marko 5:1-20. Zingatia vifungu 18-20.

ZOEZI: Jioze kusimulia hadithi yako - Unastahili kutayarisha hadithi yako na uwe umejitayarisha kuishiriki na watu wakati unawaeleza kuhusu Yesu. Unaweza kuelezea haithi yako kwa njia hii:

- Ongea kuhusu maisha yako kabla uanze kumfuata Yesu - Elezea hisia zako [machungu, upweke], maswali [kitu gani hufanyika baada ya kifo?], ama jitihadi uliyokuwa nayo kabla hujamfuata.
- Ongea jinsi ulivyofanyika mfuasi wa Yesu- Waambie kuhusu Yesu! Hadithi muhimu ya Yesu ni: Sote tumemkosea Mungu kwa dhambi zetu. Tutakufa kwa ajili ya dhambi zetu. Lakini tunaokolewa kutoka kwa kifo tukiweka imani yetu kwake Yesu, aliyefia dhambu zetu, akazikwa, na kufufuliwa kutoka wafu.
- Ongea kuhusu maisha yako baada ya kumfuata Yesu – Waelezee jinsi Yesu alivyobadilisha maisha yako. Waelezee kuhusu furaha, amani, na msamaha Yesu alikupa.
- Karibisha majibu-Hadithi yako sharti lidai majibu. Maliza kwa kuuliza swali litakalokusaidia kutambua hali ya maslahi ya kiroho ya mtu yule. Uliza kitu kama: “Je ungependa kujua jinsi unavyoweza kusamehewa?” au “Ungependa Mungu abadilishe maisha yako?”

- Acha iwe fupi [dakika 3 ama chini]- Hadithinyako iwe fupi na ya kuvutia. Usiwe wa kuchosha na usiongee sana hata msikizaji wako akapoteza hamu.

Jioze kuelezea hadithi yako na mtu mmoja katika kundi lako.

- Chagua watu 5 wa kueleza. Omba. Mwulize Mungu akuonyeshe watu 5 unaowajua na angependa uweleze kuhusu hadithi yako juma hili.

2. SIMULIA HADITHI YA YESU

ANGALIA JUU: 1 Wakorintho 15:1-8, Warumi 3:23, Warumi 6:23

ZOEZI: Acha kila mtu katika kundi lako ajizoeze kuelezea hadithi ya Yesu akitumia Mcheramba ya Uinjilisti au atumie njia nyingine rahisi. Elezea hadithi yako na hadithi ya Yesu kwa watu 5 juma hii. Fanya hivi kila juma.

3. FUATA & UVUE

ANGALIA: Marko 1:16-20

ZOEZI: Tengeneza orodha-Chukua karatasi na uandike majina ya watu mia 100 unaowajua [jamaa, marafiki, majirani, wafanya kazi wenzako au wanafunzi wenzako] Wanaohitaji kusikia kumhusu Yesu. Elezea watu 5 hadithi yako na hadithi ya Yesu juma hii. Fanya hivi kila juma.

4. UBATIZO

ANGALIA JUU: Warumi 6:3-4; Matendo 8:26-40

ZOEZI: Tafuta maji yaliyo karibu [bafu, birika, mto, ziwa] na ukabatize waumini wapya. Endelea kuwabatiza watu wanapoamini. Kujifunza mengi kuhusu ubatizo, soma Matendo 2:37-41, 8:5-13, 8:36-38, 9:10-19, 10:47-48, 16:13-15, 16:27-34, Matendo 18:5-9 na 1

Wakorintho 1:10-17, Matendo 19:1-5, Matendo 22:14-17.

Elezea watu 5 hadithi yako na hadithi ya Yesu juma hii. Fanya hivi kila juma.

1. BIBLIA

ANGALIA JUU: 2 Timotheo 3:14-16

ZOEZI: Kariri na ukasome maswali 7 za Biblia [maswali 1-7 katika muundo rahisi wa mkutano].

ONGEA NA MUNGU ANGALIA JUU: Mathayo 6:9-13

ZOEZI: Tumia mkono wako kujifunza jinsi ya kuongea na Mungu. Kama kundi ombeni sala ya Yesu katika Mathayo 6:9-13 mkitumia mikono zenu kama mwongozo.

1. **KITANGA cha MKONO = Uhusiano.**

Jinsi kitanga kilivyo msingi wa vidole vyetu na kidole cha gumba, wakati wa upweke na Mungu ni msingi wetu wa uhusiano binafsi naye. “Mungu wetu uliye mbinguni...” [Mathayo 6:9]

2. **Kidole gumba = Ibada.** Kidole gumba hutukumbusha ni lazima tumuabudu Mungu kabla ya kuomba cho chote. “...jina lako litukuzwe.” [Mathayo 6:9]

3. **Kidole cha kwanza = Kujisalimisha.** Inayofuata ni kusalimisha maisha yetu, mipango, jamaa, fedha, kazi, siku za usoni, kila kitu. “Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe...” [Mathayo 6:10]

4. **Kidole cha katikati = Ulinzi.** Tunamwuliza Mungu akutane na mahitaji zetu. “Utupe leo riziki yetu.” [Mathayo 6:11]

Kidole cha Nne = Msamaha. Sasa tumuombe Mungu atusamehe dhambi zetu, nasi lazima tuwasamehe wengine.

“Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasameheavyo wadeni wetu.” [Mathayo :12]

6. **Kidole kidogo= Ulinzi.** Kisha tunaomba ulinzi. “Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.”

[Mathayo 6:13]

7. **Kidole gumba [Tena] = Ibada.** Na tunamaliza kama tulivyoanza – tunamuabudu Mungu Mwenyezi – “ Kwa kuwa Ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.” [Mathayo 6:13].

Elezea watu 5 hadithi yako na hadithi ya Yesu juma hii. Fanya hivi kila juma.

7. NYAKATI NGUMU

ANGALIA JUU: Matendo 5:17-42; Mathayo 5:43-44

ZOEZI: Shiriki na kundi ugumu ambalo umepitia kwa ajili ya imani yako mpya; fikiria kuhusu matatizo unayoweza kukabiliana nayo; jukumu na jibu lako litakuwa nini – kwa ujasiri na upendo – kama vile Yesu anavyofundisha. Ombea mahitaji zinavyochipuka. Ombea kila mtu baada yao kushiriki.

Elezea watu 5 hadithi yako na hadithi ya Yesu juma hili. Fanya hivi kila juma.

8. KUWA KANISA

ANGALIA JUU: Matendo 2:42-47, 1 Wakorintho 11:23-34

ZOEZI: Jadilianeni kuhusu kile kundi lenu linahitaji kufanya liwe kama kanisa lililotajwa katika kifungu. Kama kundi, chora mstari dwara wenye nukta inayowakilisha kundi lako. Juu yake, orodhesha nambari 3: idadi nayohudhuria kila mara [takwimu ya kila mara], idadi inayomwamini Yesu [msalaba] na idadi baada ya kuamini [maji].



Ikiwa kundi lako limejitolea kuwa kanisa, fanya mistari yako ya nukta kuwa mraba. Ikiwa kila mara unajizoesha yafuatayo basi chora picha ya vipengele ndani ya mduara wako. Ikiwa hutafanya kulingana na vipengele au ungojee mtu wa nje aje akufanyie, kisha uchore vipengele nje ya mduara.



1. Kujitolea kuwa kanisa: Msitari imara badala ya ule wenye nukta.
2. Ubatizo-maji
3. Biblia-kitabu
4. Mkumbuke Yesu kwa mkate na kikombe-maji
5. Moyo wa-ushirika
6. Kutoa na huduma-ishara ya pesa
7. Maombi-mikono ya kuomba
8. Sifa-mikono iliyoinuliwa
9. Kuelezea watu kuhusu Yesu-rafiki akiwa ameshika mkono wa rafiki
10. aliyemuelekeza kwa imani
11. Viongozi-nyuso mbili zikitabasamu

Kundi lako linakosa nini ambacho kingeliwasaidia kufanya kanisa lenye afya?

Elezea hadithi yako na hadithi ya Yesu kwa watu 5 juma hii. Fanya hivi kila juma

KIFUATACHO NI NINI?

Angalia theluthi 3/3 Gundua njia ya theluthi 3/3 Njia ya Uwezo ama chagua kitabu cha Biblia kama Yohana au Marko [chagua tu hadithi moja kwa kila mkutano].

SAFU LA UGUNDUZI

[Kwa Vikundi Vinavyohitaji usuli wa Biblia & Uzoefu]

Tumia vifungu vifuatavyo kwa

“ANGALIA JUU” sehemu ya kundi lako. Huenda kundi lako litahitaji mkutano zaidi wa mara moja kwa vifunguo.

Mgundue Mungu-Je, Mungu ni nani na anafanana aje

1. Uumbaji-Mwanzo 1
2. Uumbaji wa wanadamu Mwanzo 2
3. Uasi wa watu-Mwanzo 3
4. Nuhu na mafuriko-Mwanzo 6:5-8:14
5. Ahadi ya Mungu na Nuhu Mwanzo 8:15-9:17
6. Mungu anaongea na Ibrahimu-Mwanzo 12:1-7; 15:1-6
7. Daudi kawa mfalme wa kizazi cha Ibrahimu-1 Samweli 16:1-13; 2 Samweli 7:1-28
8. Mfalme Daudi na Bathsheba-2 Samweli 11:1-27
9. Hadithi ya Nathani -2 Samweli 12:1-25

10. Mungu anaahidi Mwokozi atakuja-Isaya 53

Mgundue Yesu-Yesu ni nani na kwa nini alikuja

1. Mwokozi anazaliwa-Mathayo 1:18-25
2. Ubatizo wa Yesu-Mathayo 3:7-9, 13-15
3. kuponywa kwa mtu aliyepagawa-Marko 5:1-20
4. Yesu hampotezi kondoo-Yohana 10:1-30
5. Yesu amponya kipofu-Luka 18:31-42
6. Yesu na Zakayo-Luka 19:1-9
7. Yesu na Mathayo-Mathayo 9:9-13
8. Yesu ndiye njia ya pekee-Yohana 14:1-15
9. Kuja kwa Roho Mtakatifu-Yohana 16:5-15
10. Meza ya Bwana-Luka 22:14-20
11. Kukamatwa na kushitakiwa-Luka 22:47-53; 23:13-24
12. Kuuawa-Luka 23:33-56
13. Yesu yu hai-Luka 24:1-7, 36-47; Matendo 1:1-11
14. Kuamini na kutenda-Wafilipi 3:3-9

SAFU YA UWEZO

[Kwa Waumini Wsapya au Makundi yanayohitaji Mtazamo wa Uanafunzi]

Yesu Anasema-jifunze kutii amri za kimsingi za Yesu. Endelea kumshiriki Yesu na watu walio kwenye orodha yako.

1. Jifunze na utende-Yohana 14:15-21!
2. Tubu. Amini. Fuata. Marko 1:14-17, Waefeso 2:1-10
3. Ukabatizwe-Mathayo 28:19, Matendo 8:26-38
4. Mpende Mungu. Penda watu-Luka 10:25-37

Yesu pia anasema-jifunze kutii amri za kimsingi za Yesu. Endelea kumshirikisha Yesu na watu walio katika orodha yako.

1. Ongea na Mungu-Mathayo 6:9-13. Jifunze na ukajizoeshe mfano wa maombi ya Yesu
2. Kumbuka na ukamuadhimishe Yesu -Luka 22:14-20, 1 Wakorintho 11:23-32
3. Toa-Matendo 4:32-37
4. Pitisha-Mathayo 28:18-20

Fuata jinsi ninavyofuata-Fanya wanafunzi. Pitishia wengine yale mmejifunza. Fundisha hawa watu nao wapitishie.

1. Pata mwanafunzi-2 Timotheo 1:1-14
2. Pitisha-2 Timotheo 2:1-4, 14-16
3. Wafundishe kufundisha wengine-2 Timotheo 3:1-17 3.4 Nyakati ngumu-2 Timotheo 4:1-22

Zidisha Kundi lako la Theluthi 3/3 Wakusanye wanafunzi wako kuwa makundi mapya. .

1. Anza na uwe na mpango-Luka 10:1-11. Sikiza maagizo ya Yesu wakati unapoanzisha kundi jipya.
2. Kusanyikeni-Matendo 2:14-47
3. Mtu wa amani-Marko 5:1-20, 6:53-56. Tafuta watu wanaotaka kushiriki hadithi zao kumhusu Yesu. Anzisha kundi na mtu yule & na marafiki zake & jamaa.
4. Nani yuko tayari-Mathayo 13:1-9, 18-23

Ongoza-jifunze jinsi ya kuongoza kundi la theluthi 3/3.

1. Mfano [ongoza hivi]-Yohana 13:1-17
 2. Mfano [usioongoze jinsi hii]-3 Yohana 5-14
 3. Saidia-Marko 4:35-41
- 5.4 Anaglia**-Luka 10:1-11, 17, 20
5.5 Acha-Mathayo 25:14-30

Enda: mtaani-jifunze jinsi ya kufikia jamii yako.

- 6.1** Go: local-Acts 1:1-8
- 6.2** Help the poor. Share the good news- Luke 7:11-23
- 6.3** Go where God sends-Acts 10:9-48
- 6.4** Go with a plan-Acts 13:1-3, 32-33, 38-39; 4:21-23, 26-27

Go: global-learn how to reach the ends of the earth.

- 7.1** Go: global-Acts 1:1-8, Matthew 28:19-20
- 7.2** Go where God sends-Acts 8:26-38
- 7.3** God loves every people group-John 4:4-30, 39-41 7.4 Go with a plan-Acts 13:1-3, 32-33, 38-39; 14:21-23, 26-27

Remember the basics. Learn what to do when you meet.

- 8.1** Jesus is First-Philippians 2:1-11
- 8.2** Talk with God-Matthew 6:9-13
- 8.3** Community-Hebrews 10:23-25
- 8.4** The Bible-2 Timothy 3:10-17

Commit-learn to stay strong and keep following Jesus.

- 9.1** Disobedience-Jonah 1
- 9.2** Commit-Jonah 2
- 9.3** Obey-Jonah 3
- 9.4** Obey all the way-Jonah 4
- 9.5** Use it or Lose it-Matthew 25:14-30

WHERE NEXT?

Choose your own Bible passages and keep meeting. Use the same questions and group meeting format. Don't stop meeting.



wanafunzi wanaojizidisha